**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI, MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR ILIYOTOLEWA KATIKA KILELE CHA SIKU YA SHERIA (LAW DAY), TAREHE 9 FEBRUARI, 2026**

---

**MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI, RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI NA MGENI RASMI WA SHUGHULI YETU YA LEO;**

**MHESHIMIWA KHAMIS RAMADHAN ABDALLA, JAJI MKUU WA ZANZIBAR;**

**MHESHIMIWA GEORGE M. MASAJU, JAJI MKUU WA TANZANIA;**

**MHESHIMIWA ZUBEIR ALI MAULID, SPIKA WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR;**

**MHESHIMIWA DKT. MWALIMU HAROUN ALI SULEIMAN, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA;**

**MHESHIMIWA DKT. MUSTAFA SIYANI, JAJI KIONGOZI, MAHAKAMA KUU YA TANZANIA;**

**WAHESHIMIWA MAJAJI WA MAHAKAMA KUU;**

**MHESHIMIWA KADHI MKUU WA ZANZIBAR;**

**MHESHIMIWA NAIBU KADHI MKUU;**

**MHESHIMIWA KATIBU WA BARAZA LA MAPINDUZI NA KATIBU MKUU KIONGOZI;**

**MHESHIMIWA MRAJIS WA MAHAKAMA KUU ZANZIBAR;**

**MTENDAJI MKUU WA MAHAKAMA KUU ZANZIBAR;**

**WAHESHIMIWA MAWAZIRI;**

**MHESHIMIWA MKUU WA MKOA WA KASKAZINI PEMBA;**

**MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR;**

**RAIS WA JUMUIYA YA WANASHERIA ZANZIBAR;**

**KATIBU MKUU, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA;**

**WAKUU WA TAASISI MBALI MBALI;**

**WAKUU WA VYOMBO VYA ULINZI NA USALAMA;**

**WAHESHIMIWA VIONGOZI WA DINI;**

**MAWAKILI WOTE MLIOHUDHURIA, KUTOKA AFISI YA MWANASHERIA MKUU, AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA PAMOJA NA MAWAKILI WA KUJITEGEMEA;**

**WAFANYAKAZI NA WATENDAJI WOTE WA MAHAKAMA MLIOHUDHURIA;**

**WAGENI WAALIKWA – MABIBI NA MABWANA;**

**ITIFAKI IMEZINGATIWA.**

**ASSALAM ALAYKUM WARAHMATULLAH WABARAKATUH**.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**
Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kuungana na wenzangu walionitangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kushiriki na kushuhudia kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar.

Aidha, kwa namna ya kipekee, napenda nimshukuru Mheshimiwa Khamis Ramadhan Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa kunialika na kunipa fursa hii adhimu ya kutoa salamu pamoja na maelezo mafupi yenye mnasaba na siku hii ya leo. Fursa hii inaakisi dhamira

ya dhati ya uongozi wa Mahakama ya Zanzibar katika kuimarisha mshikamano na taasisi za haki na kuendeleza misingi ya utawala wa sheria katika nchi yetu.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Ninapenda kutumia fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa kipindi cha pili. Kupitia uongozi wake, Serikali imeendelea kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha utekelezaji wa sera, mipango na programu za maendeleo kwa lengo la kufikia maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi wote wa Zanzibar.

Kwa dhati kabisa, tunaipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wake kwa kuendelea kuweka kipaumbele stahiki kwa Mahakama pamoja na wadau wake wote kwa kuwawekea mazingira bora kabisa ya kazi, kuanzia miundombinu, vitendea kazi pamoja na maslahi bora kwa watendaji wake.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Aidha, ninapenda nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu, Mheshimiwa Kadhi Mkuu, Mrajis, Mahakimu, Makadhi, Watendaji na Watumishi wote wa Mahakama, Mawakili wa Serikali na wa Kujitegemea pamoja na Wadau wote wa Mahakama kwa jitihada zao

kubwa katika kusimamia haki pamoja na kuweka misingi imara ya mashirikiano.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Kauli Mbiu ya Mwaka huu inayosema **"Maboresho ya Mfumo wa TEHAMA kwa Taasisi za Sheria ni chachu katika utoaji wa haki kwa jamii"** kwa hakika inaakisi mwelekeo sahihi wa maboresho katika sekta ya haki. Ni dhahiri kuwa, kauli mbiu hii inasadifu moja kwa moja kauli ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa wakati wa uzinduzi na hotuba yake kwa Baraza la Kumi na Moja la Wawakilishi tarehe 10 Novemba, 2025, aliposisitiza umuhimu wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kurahisisha na kuimarisha utoaji wa haki kwa jamii. Kauli mbiu hii inaendana na dhamira ya dhati ya Serikali katika kuweka na kusimamia misingi imara ya matumizi ya teknolojia kama nyenzo muhimu ya kufanikisha upatikanaji wa haki kwa wananchi wote bila kujali tofauti zao za kijamii, kiuchumi au kimaeneo.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Kwa kuzingatia kauli mbiu hii, ni imani yangu kuwa kila mmoja wetu ataizingatia kwa umakini kwa lengo la kujitathmini na hivyo kuweza kuyafikia matarajio ya taifa letu katika kuweka misingi imara ya Utawala wa Sheria na upatikanaji wa haki kwa kila mwanachi kwa kuzingatia uwepo wa maboresho ya mifumo ya TEHAMA katika Taasisi zetu za Sheria**.**

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Kwa mwaka 2025, Afisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoja na majukumu mengine, imeendelea kuiwakilisha Serikali na taasisi zake katika mashauri mbali mbali ya madai yanayoendelea katika Mahakama. Aidha, Afisi imeendelea kutoa huduma za ushauri wa kisheria kwa wananchi wanaofika Afisini kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya Serikali na taasisi zake.

Vilevile, Afisi inaendelea kusimamia na kutoa ushauri wa kisheria kuhusu mikataba inayofungwa kwa niaba ya Serikali, sambamba na kufanya mapitio na tafiti za sheria mbali mbali za Zanzibar.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa kauli mbiu ya Maboresho ya Mfumo wa TEHAMA kwa Taasisi za Sheria, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imenunua vifaa vya mfumo wa kieletroniki kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Afisi. Kwa sasa, Afisi ipo katika hatua za mwisho za kumpata Mshauri Elekezi atakayesimamia uandaaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu na kusimamia hatua muhimu za utekelezaji wa majukumu ya Afisi. Mfumo huo unatarajiwa kurahisisha na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Kwa hatua ya awali, mfumo huo utahusisha taarifa muhimu za Mawakili wa Serikali wanaofanya kazi au wanaosimamiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoja na kuweka kumbukumbu za hatua mbali mbali zinazopitiwa katika mikataba ya Serikali na kazi nyengine zinazofanywa na Afisi yetu.

Kutokana na kukamilika kwa tovuti rasmi ya Afisi, hivi karibuni Afisi itaziweka Sheria zote za Zanzibar zilizokusanywa kwa njia ya nakala laini, kuanzia mwaka 1908 hadi kufikia 2025. Hatua hiyo itawawezesha wadau wote wa sheria pamoja na wananchi kwa ujumla kuweza kuzitumia sheria hizo katika shughuli zao mbali mbali.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Katika hatua za kujiwekea taratibu za kazi zinazoeleweka na kutekelezeka kwa umakini na ufanisi, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa Miongozo ya Kiutendaji (Manuals). Kwa kuanzia, Afisi imechapisha na kusambaza Muongozo wa Uandishi wa Sheria ambao unatoa maelezo na utaratibu mzima wa uandishi wa sheria na kanuni nchini. Aidha, Muungozo huu utasaidia Taasisi zilizo nje ya Afisi kufahamu misingi mikuu inayotakiwa kufuatwa katika uandishi wa sheria na kanuni za nchi.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha na kuhuisha sekta ya sheria nchini. Katika mwelekeo huo, Afisi inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu Namba 6 ya 2013, kwa lengo la kuwaweka Maafisa Sheria na Mawakili wa wote wa Serikali ukiachia wale ambao wameainishwa vyenginevyo na sheria kuwa chini ya usimamizi wa Mwanasheria Mkuu.

Dhamira kuu ya hatua hii ni kuimarisha malezi ya kitaaluma, kuwajengea uwezo, na kuwaongezea ujuzi Mawakili na Maafisa Sheria wa Serikali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na kwa kuzingatia misingi ya utawala wa sheria.

Katika hatua nyengine muhimu, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imefanikiwa kuwateua na kuwatangaza Maafisa Sheria kumi na tano (15), kutoka taasisi mbali mbali za Serikali kuwa Mawakili wa Serikali kwa kuzingatia muda wao wa utumishi pamoja na uzoefu wao katika kazi za kisheria. Uteuzi huu una lengo la kuwawezesha Mawakili wa Serikali hao kutambuliwa rasmi, kupata usimamizi na msaada unaostahiki kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilifanya mapitio ya Sheria Saba (7) zilizofikia hatua mbali mbali za utafiti. Afisi pia imefanikiwa kuandaa Sheria tatu (3) mbali mbali kwa lugha nyepesi. Aidha, Afisi imejiwekea utaratibu maalumu unaoiwezesha kuandaa vipindi na programu mbali mbali katika vituo vya redio na televisheni pamoja na kuwafikia wananchi katika Shehia mbali mbali Unguja na Pemba na kuweza kuwapatia elimu ya sheria.

Hatua hii inakwenda sambamba na Mpango wa Maendeleo – Zanzibar (ZADEP) 2021-2026 ambapo Serikali imeazimia kwamba ifikapo mwaka 2026 kuongeza kwa asilimia thelathini na tano (35%)

idadi ya watu wanaopatiwa huduma ya msaada wa kisheria bila ya kuwepo kwa ubaguzi wowote.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

Katika hatua za kuongeza uelewa wa sheria kwa watendaji wa Afisi na jamii kwa ujumla, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imekuja na mkakati wa kutayarisha na kuchapisha ripoti ya tathmini ya sheria kwa kila mwaka. Kwa kuanzia, Afisi imefanikiwa kuchapisha Tathmini ya Mapitio ya Sheria (Toleo la Mwaka 2024). Tathmini hii inatoa muhtasari wa sheria na kanuni muhimu za Zanzibar zilizopitishwa kwa mwaka 2024. Aidha, ufanyaji wa tathmini hiyo umefuata uzoefu wa nchi nyengine nje ya Zanzibar katika taratibu za kufanya mapitio ya sheria, sambamba na kuonesha umuhimu wa kutumia maamuzi ya kesi na kuifahamu mikataba ya kikanda na kimataifa.

**MHESHIMIWA MGENI RASMI,**

**Kwa kuhitimisha**, napenda kuwakumbusha wadau na wananchi wote juu ya umuhimu wa kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano hapa nchini, sambamba na kutimiza wajibu wetu kila mmoja kwa mujibu wa sheria na misingi ya utawala bora.

Mwisho kabisa, kwa mara nyengine tena napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kutoa salamu pamoja na maelezo

yangu katika maadhimisho haya muhimu ya Siku ya Sheria Zanzibar.

**Nawashukuru kwa kunisikiliza.**

***AHSANTENI SANA.***